NEW VINE CHURCH -HQ
GREATER GLORY CONFERENCE 14/08/2025 - "SUPERNATURAL TURN AROUND"
SOMO: **KUHUSIKA KWAKO KUKO VIPI (HOW IS YOUR INVOLVMENT)?**
APOSTLE ISACC NGANGA

1 Samweli 2:30 "*Kwa sababu hiyo, BWANA, Mungu wa Israeli, asema, Ni kweli, nalisema ya kuwa nyumba yako, na nyumba ya baba yako itakwenda mbele zangu milele; lakini sasa BWANA asema, Jambo hili na liwe mbali nami; kwa maana wao wanaoniheshimu nitawaheshimu, na wao wanaonidharau watahesabiwa kuwa si kitu.*"

Mungu anaangalia mwanadamu anahusikaje kwenye jambo kabla yeye mwenyewe hajahusika; kuhusika kwa mwanadamu kuna aamua namna Mungu atahusika.

Kutoka 3:3 "*Musa akasema, Nitageuka sasa, niyaone maono haya makubwa, na sababu kijiti hiki hakiteketei.*"

Mungu alianza kusema na Musa baada ya Kusa kugeuka ili ayaone maono makubwa ambayo Mungu alikua ampe.

Mungu huwaheshimu wanaomheshimu na wale wanamdharau anawadharau; kumdharau Mungu ni kuwa mwovu mbele za Mungu,

Makuhani walihusika na sanduku la agano; kila mwamini anapaswa kujua ni kwa namna gani anahusika na sanduku la agano ili anaufaike;

Uhusika wa makuhani katika Sanduku la agano

Makundi matano ya watu waliohusika na sanduku la agano na yaliyotokea
1. Kuhani Eli na wanae
1 Samweli 2:12-17 "*Basi, hao wana wa Eli walikuwa watu wasiofaa kitu; hawakumjali BWANA, wala haki ya makuhani ilivyokuwa kwa watu. Wakati huo mtu ye yote alipotoa dhabihu wakati wo wote, ndipo huja mtumishi wa kuhani, nyama ilipokuwa katika kutokota, naye akawa na uma wa meno matatu mkononi mwake; naye huutia kwa nguvu humo chunguni, au birikani, au sufuriani, au chomboni; nyama yote iliyoinuliwa kwa huo uma kuhani huichukua mwenyewe. Ndivyo walivyofanya huko Shilo kwa Waisraeli wote waliokuja huko. Tena, kabla ya kuteketeza mafuta, huja mtumishi wa kuhani, akamwambia yule mwenye kuitoa dhabihu, Mtolee kuhani nyama ya kuoka; kwa kuwa hataki kupewa nyama iliyotokoswa, bali nyama mbichi. Tena, ikiwa mtu yule amwambia, Hawakosi wataichoma moto hayo mafuta kwanza, kisha utwae kadiri roho yako itakavyoopenda; ndipo husema, Sivyo, lakini sharti unipe sasa hivi; la, hunipi, basi nitaitwaa kwa nguvu. Hivyo dhambi yao wale vijana ilikuwa kubwa sana machoni pa BWANA; kwa maana hao watu walidharau sadaka ya BWANA.*"

1 Samweli 4:10-22 "*Wafilisti wakapigana nao, Israeli wakapigwa, wakakimbia kila mtu hemani kwake; wakauawa watu wengi sana; maana katika Israeli walianguka watu thelathini elfu wenye kwenda vitani kwa miguu. Hilo sanduku la Mungu Likatwaliwa; na Hofni na Finehasi, wale wana wawili wa Eli, wakauawa. Basi, mtu mmoja wa Benyamini akapiga mbio kutoka mle jeshini akafika Shilo siku ile ile, hali nguo zake zimeraruliwa, na mavumbi kichwani mwake. Alipofika, tazama, Eli alikuwa ameketi kitini pake kando ya njia, akingojea; maana moyo wake ulitetemeka kwa ajili ya sanduku la Mungu. Na yule mtu alipoingia mjini, akatoa habari, mji wote ukalia.Naye Eli aliposikia kelele za kile kilio, akasema, Maana yake nini kelele za kishindo hiki? Yule mtu akafanya haraka, akaenda, akamwambia Eli. Basi Eli umri wake umepata miaka tisini na minane; na macho yake yamepofuka hata asiweze kuona. Yule mtu akamwambia Eli, Mimi ndimi niliyetoka jeshini, nami leo hivi nimekimbia toka jeshini. Naye akasema, Yalikwendaje, mwanangu? Yeye aliyeleta habari akajibu, akasema, Israeli wamekimbia mbele ya Wafilisti, tena watu wengi sana wameuawa, hata na wana wako wawili, Hofni na Finehasi, wamekufa pia, na sanduku la Mungu limetwaliwa. Ikawa alipolitaja sanduku la Mungu, Eli akaanguka kitini pake kwa nyuma, kando ya mlango, shingo yake ikavunjika, akafa; maana alikuwa mzee, tena mzito. Naye alikuwa amewaamua Israeli miaka arobaini. Tena mkwewe, mkewe huyo Finehasi, alikuwa mja-mzito,*

*karibu na kuzaa; basi, aliposikia habari ya kutwaliwa sanduku la Mungu, na ya kwamba mkwewe na mumewe wamekufa, akajiinamisha, akazaa; maana utungu wake ulimfikilia. Hata alipokuwa katika kufa, wale wanawake waliohudhuria karibu naye wakamwambia, Usiogope; kwa maana umezaa mtoto mwanamume. Walakini hakujibu, wala hakumtazama."*

Wana wa Eli walikua wanalihudumu sanduku la agano, lakini walichagua kumdharau Mungu kwa kufanya uovu katika hekalu na mbele ya sanduku la agano; Eli alishindwa kuonya na kuandaa makuhani ambao wangepelekea heshima ya sanduku la agano; Eli na familia yake walipata adhabu kwa sababu walihusika kwenye kupelekea utukufu wa Mungu kupotea.

2. **Wafilisti**
1 Samweli 5:1-6 *"Basi Wafilisti walikuwa wamelichukua sanduku la Mungu, wakaenda nalo kutoka Eben-ezeri hata Ashdodi. Wafilisti wakalichukua sanduku la Mungu, wakalitia katika nyumba ya Dagoni, wakaliweka karibu na Dagoni. Na watu wa Ashdodi, walipoamka alfajiri siku ya pili, kumbe! Dagoni imeanguka chini kifudifudi, mbele ya sanduku la BWANA. Wakaitwaa Dagoni, wakaisimamisha mahali pake tena. Hata walipoamka kesho yake asubuhi, kumbe! Dagoni ilikuwa imeanguka chini kifudifudi, mbele ya sanduku la BWANA; na kichwa chake Dagoni na vitanga vya mikono yake vyote viwili vimekatika, vipo vimelala kizingitini; Dagoni ikasalia kiwiliwili chake tu. Kwa hiyo makuhani wa Dagoni, na mtu awaye yote aingiaye nyumbani mwa Dagoni, hawakanyagi kizingiti cha nyumba ya Dagoni huko Ashdodi, hata leo. Lakini mkono wa BWANA ulikuwa mzito juu ya watu wa Ashdodi, akawaharibu, akawapiga kwa majipu, huko Ashdodi na mipakani mwake."*

Wafilisti walichukua sanduku la Mungu na kulichanganya na miungu yao; hii inahusika moja kwa moja na roho ya changanyachanganya; unaweza ukasikia mtu huyo ni mcha Mungu lakini ana mambo mengine yanayomchukiza Mungu.

Mkono wa Mungu huwapiga wote wanaochanganya sanduku la agano yaani utukufu wa Mungu na mambo mengine yanayomchukiza na kumdharau Mungu.

3. **Abinadabu na nyumba yake**
1 Samweli 7:1-2 *"Na hao watu wa Kiriath-yearimu wakaja, wakalichukua sanduku la BWANA, wakalileta ndani ya nyumba ya Abinadabu huko kilimani, nao wakamtenga Eleazari, mwanawe, ili alilinde sanduku la BWANA. Ikawa, tangu siku hiyo ambayo sanduku lilikaa Kiriath-yearimu wakati ulikuwa mwingi; kwa maana ulikuwa miaka ishirini; na nyumba yote ya Israeli wakamwombolezea BWANA."*

Hakuna jambo ambalo lilibadilika wakati sanduku la Bwana lilikuwa nyumbani mwa Abinadabu kwa miaka ishirini, sanduku lile lile lililokua linawapiga wafilisti, hakuna taarifa inayoonyesha badiliko lililotokea kwenye nyumba ya Abinadabu.

Mtu anaweza akakaa kanisani kwa muda mrefu sana na hakuna chochote kinabadilika kwenye maisha yake kwa sababu anashindwa kuhusika vizuri kwenye neema na uwepo wa nguvu za Mungu kwenye kanisa alilopo.

Namna tunavyohusika na uwepo wa Mungu inaamua sana namna Mungu atahusika nasi kwenye maeneo yote ya maisha yetu.

4. **Uza na Sanduku la agano**
2 Samweli 6:1-8 *"Basi Daudi akakusanya tena wateule wote wa Israeli, watu thelathini elfu. Akaondoka Daudi akaenda pamoja na watu wote waliokuwa naye, mpaka Baala wa Yuda, ili kulipandisha kutoka huko sanduku la Mungu lililoitwa kwa jina, naam, jina la BWANA wa majeshi akaaye juu ya makerubi. Wakaliweka sanduku la Mungu juu ya gari jipya, wakalitoa katika nyumba ya Abinadabu, iliyoko kilimani; nao Uza na Ahio wana wa Abinadabu wakaliendesha lile gari jipya. Wakalitoa katika nyumba ya Abinadabu iliyoko kilimani, pamoja na sanduku la BWANA; na huyo Ahio akatangulia mbele ya sanduku. Daudi na nyumba yote ya Israeli wakacheza mbele za BWANA kwa nguvu zao zote, kwa nyimbo, na kwa vinubi, na kwa vinanda, na kwa matari, na kwa kayamba, na kwa matoazi. Hata walipofika kwa uga ya Nakoni, Uza*

*akalinyoshea mkono sanduku la Mungu, akalikamata kwa maana wale ng'ombe walikunguwaa. Ndipo hasira ya BWANA ikawaka juu ya Uza; naye Mungu akampiga huko kwa kosa lake; hata akafa pale pale penye sanduku la Mungu. Daudi akaona uchungu kwa kuwa BWANA amemfurikia Uza; akapaita mahali pale Peres-uza hata leo."*

Mgeuko wa jambo lolote kwenye maisha yako halitaku

Kosa la Uza;
a. Sanduku la Mungu halikutakiwa kuwekwa kwenye gari, kwa sababu sanduku la agano lilitakiwa kubebwa kwenye mabega ya makuhani

Kuna mambo ambayo huwezi kuya delegate

b. Kuligusa sanduku la agano ilikua ni kuugusa utukufu wa Mungu kwa mikono ya nyama; usa kama kuhani alishindwa kuzingatia itifaki ya kuhamisha sanduku la agano; mambo katika nyumba ya Mungu.

Unaweza kuwa na nia nzuri, lakini itifaki hauna, kwenye nyumba ya Mungu; nyumba ya Mungu ina nidhamu yake, sio nyumba iliyochanganyikiwa.

Namna za kuhusika katika uwepo wa Mungu ni kuhakikisha unatekeleza wajibu wako kama Mungu mwenyewe anavyotaka kwenye mambo ya Mungu

5. **Obed-edomu**
2 Samweli 6:9-12 *"Naye Daudi akamwogopa BWANA siku ile; akasema, Litanijiaje sanduku la BWANA? Basi Daudi hakutaka kulileta sanduku la BWANA kwake mjini mwa Daudi; ila Daudi akalihamisha nyumbani kwa Obed-edomu, Mgiti. Sanduku la BWANA akalitia katika nyumba ya Obed-edomu, Mgiti, muda wa miezi mitatu; naye BWANA akambarikia Obed-edomu, na nyumba yake yote. Kisha mfalme Daudi akaambiwa ya kwamba, BWANA ameibarikia nyumba ya Obed-edomu, na vitu vyote alivyo navyo kwa ajili ya sanduku la Mungu. Daudi akaenda, akalileta sanduku la Mungu, toka nyumba ya Obed-edomu mpaka mji wa Daudi, kwa shangwe."*

Obed-edom alipata kufanikiwa kwa kuwa aliamua kuhusika kwenye kulitunza sanduku la agano kwa heshima na kwa namna njema zaidi (2 Samweli 6:9-12)